WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA AWALI NA MAFUNZO YA UFUNDI
KAZI YA RIKIZO MEI 2020
KISWAHILI VII

JINA: _____ TAREHE: _____

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A,B,C,D,na E yenye maswali 45
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu
3. Maswali 1-40 ni ya kuchagua. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye kisanduku pembeni Maswali 41-45 uyajibu kwa majibu ya kujieleza kwa ufupi
4. Mwandiko mzuri ulio wazi utakupatia alama halali

SEHEMU A: SARUFI

1. Wingi wa sentensi 'ng'ombe wangu alizaa' ni upi?_____
   (a) Ng'ombe zangu zilizaa
   (b) Ng'ombe wangu walizaa
   (c) Ng'ombe zao zilizaa
   (d) Ng'ombe wetu alizaa
   (e) Ng'ombe wetu walizaa
   ( )

2. Acha kufanya jambo kwa kuofia litaleta matokea mabaya. Neno lipi kati ya yafuatayo lina maana ya maelezo hayo.
   (a) Ukungu
   (b) Huzuni
   (c) Chelea
   (d) Farijika
   (e) Hasira
   ( )

3. Kamilisha sentensi ifuatayo kwa neno stahili.
   "Mama _____majonzi kwa kufiwa na mtoto wake.
   (a) Alihisi
   (b) Alikuwa na
   (c) Alisikia
   (d) Aliona
   (e) Alijifariji
   ( )

4. Kati ya maneno yafuatayo ni lipi lisilohhusiana na mengine:_____
   (a) Kanchiri
   (b) Suruali
   (c) Kofia
   (d) Kaptura
   (e) Kanzu
   ( )

5. Mama atapika chakula katika sentensi hiyo kiambishi cha wakati ni kipi kati ya vifuatavyo;
   (a) –ma –
   (b) –ku-
   (c) –ta-
   (d) –ni-
   (e) Cha-
   ( )

6. Wapishi hupika chakula cha wanafunzi wote. Kitenzi cha sentensi hiyo kiko katika hali gani?
   (a) Mazoea
   (b) Kuendelea
   (c) Timilifu
   (d) Sasa
   (e) Iliyopita
   ( )

( )

7. Nilicheza mpira uwanjani kwa nud wa kutosha. Sentensi hiyo ni ya nafsi ipi?____
   (a) Nafsi ya kwanza
   (b) Nafsi ya pili
   (c) Nafsi ya tatu umoja
   (d) Nafsi ya tatu
   (e) Nafsi ya kwanza wingi

8. Hawakufanya mgomo wowote. Kipi ni kiambishi cha nafsi katika sentensi hiyo_____
   (a) –wa-
   (b) Ha-
   (c) –ku-
   (d) –fa-
   (e) –te-

9. Katika neno "wanamtukuza," kiambishi cha nafsi mtendwa ni kipi?_____
   (a) Wa-
   (b) –tu-
   (c) –na-
   (d) –m-
   (e) –ku-

10. Ni seti ipi ya maneno iko katika ngeli ya U-I_____
   (a) Meza, kalamu, nguo
   (b) Airisha, papai, jipu
   (c) Mti, mlango, mkoba
   (d) Kitabu, chungu, kiti
   (e) Ukuta, ungo, ufagio
   ( )

11. Uyakinishi wa neno " usichelewe" ni _____
   (a) Chelewa
   (b) Achelewe
   (c) Cheleweshwa
   (d) Usije
   (e) Uwahi
   ( )

12. Wazazi wake wanaishi <u>karibu ya shule yetu</u> kifungu cha maneno kilichopigiwa mstari kimetumika kama _____
   (a) Kivumishi
   (b) Kiunganishi
   (c) Kielezi
   (d) Kihisishi
   (e) Kitenzi
   ( )

13. Kelele anayotoa mtu anayeomba msaada ni yowe au _____
   (a) Kilele
   (b) Kigelegele
   (c) Mluzi
   (d) Nduru
   (e) Ukulele
   ( )

14. Kisawe cha mvivu ni _____
   (a) Kegelege
   (b) Mnyonge
   (c) Mzembe
   (d) Kakamavu
   (e) Hodari
   ( )

15. Mahali pasipo mvua, majani wala miti ni _____
   (a) Bahari
   (b) Mjini
   (c) Barabara
   (d) Jangwa
   (e) Milima
   ( )

16. Sisi tulifukia takataka sentensi hiyo iko katika kauli ipi?_____ ( )
    (a) Kutendeka
    (b) Kutenda
    (c) Kutendea
    (d) Kutendana
    (e) Kutendesha

17. Bwana shamba wetu alizindua mbegu bora. Katika sentensi hiyo kitenzi katika sentensi hiyo ni _____ ( )
    (a) Shamba
    (b) Mbegu
    (c) Bora
    (d) Alizindua
    (e) Wetu

18. Mbwa huyu anabweka vibaya. Neno vibaya katika sentensi hiyo limetumika kama;- ( )
    (a) Kielezi
    (b) Kivumishi
    (c) Kitenzi
    (d) Nomino
    (e) Kiunganishi

19. Mtoto mlafi amepaliw <u>na</u> chakula. Neno lililopigiwa mstari ni _____ ( )
    (a) Kitenzi shirikishi
    (b) Kivumishi cha A-unganifu
    (c) Kiunganishi
    (d) Kitenzi
    (e) Nomino

20. <u>Kulia</u> kwake ni kicheko kwetu. Neno lililopigiwa mstari limetumika kama aina ipi ya nomino. ( )
    (a) Nomino
    (b) Kitenzi
    (c) Kinyume
    (d) Kula
    (e) Kiwakilishi

SEHEMU B: LUGHA YA KIFASIHI

21. Chungulia kaburi ni nahau yenye maana sawa na nahau ipi kati ya zifuatazo_____ ( )
    (a) Gofu la mtu
    (b) Tia chumvi
    (c) Oga dunia
    (d) Ponea chupachupa
    (e) Shikwa na homa

22. Ukimtoa nje hufa. Jibu la kitendawili hiki ni _____ ( )
    (a) Mjusi
    (b) Yai
    (c) Kuku
    (d) Samaki
    (e) Nguo

23. <u>Mioyo yao ilifinywa</u> baada ya kukosa kile walichokitegemea. Nini maana ya nahau iliyopigiwa mstari_____ ( )
    (a) Walisikitishwa
    (b) Waliumia
    (c) Walikimbia
    (d) Walisamehe
    (e) Walihofu

24. Mama hachoki kunibeba ni kitendawili kilicho na maana iliyo sawa na kitendawili kipi kati ya vifuatavyo_____
    (a) Ubwabwa wa mwana mtamu
    (b) Mama nieleke
    (c) Gari langu halitumii mafuta ya waarabu
    (d) Hausimami hausimiki
    (e) Amefika kabla mjumbe hajarudi
    ( )

25. Kamilisha methali "Paka akiondoka _____
    (a) Panya huvizia
    (b) Ndipo painukapo
    (c) Panya hutawala
    (d) Hapaingii panya
    (e) Panya hujificha shimoni
    ( )

26. Njia ya mwongo ni fupi. Methali ipi kati ya zifuatazo ina maana inayolandana na hiyo._____
    (a) Mbio za sakafuni huishia ukingoni
    (b) Mtaka yote kwa pupa hukosa yote
    (c) Mla ni mla deo, mla jana kala nini?
    (d) Nyama ya ulimi ni tamu
    (e) Ngozi ivute ili maji
    ( )

27. Methali ipi kati ya zifuatazo ni kinyume cha methali, "si vyote ving'aavyo ni dhahabu"
    (a) Subira yavuta heri
    (b) Mvunja nchi ni mwananchi
    (c) Dalili ya mvua ni mawingu
    (d) Haraka haraka haina Baraka
    (e) Mtoto mkaidi afaidi mpka siku idi
    ( )

28. Babu anapiga mbizi, akiibuka ndevu zimekuwa nyeupe. Kitendawili hicho kinateguliwa kwa jibu lipi?_____
    (a) Mwiba
    (b) Mwiko
    (c) Mkono
    (d) Taa
    (e) Nyota
    ( )

29. Alipofika uwanjani, alimkuta mtu wa miraba minne. "mtu wa miraba minne maana yake ni ipi?_____
    (a) Mtu mwenye shati la miraba minne
    (b) Mtu aliyechora miraba minne
    (c) Mtu mfupi na mnene
    (d) Mtu mnene na mwenye nguvu
    (e) Mtu mwembamba asiye na nguvu
    ( )

30. Visha kilemba cha ukoka ni nahau inayolandana katika maana na nahau isemayo;-
    (a) Piga chuku
    (b) Kufa moyo
    (c) Piga mtindi
    (d) Zunguka mbuyu
    (e) Paka mafuta kwa mgongo wa chupa
    ( )

SEHEMU C: USHAIRI

Soma shairi lifuatalo na kisha jibu maswali

Maua kwa uhakika, ni mapambo ya dunia,
Yatazame kila mwaka, lazima yatachanua,
Ni wakati wa masika, mbeguze huzifumua.

Miche nayo inatoka, ikaanza kuchipua,
Mvua ikianguka, huendelea kukua,
Hata kimo kikifika, utayaona maua.

Mlangoni ukitoka, linapochomoza jua,
Utataka kuondoka, macho yalivyokutua,
Kuyakata utataka, mikononi kuchukua.

Pengine utayafyeka, ukutani kuyatia,
Mezani pia kuweka, jioni ikifikia,
Yote yameshakauka, ukijisikitikia.

Kama kweli wayataka, mbona wayashambulia?
Lazima yatakauka, mtini ukiyatoa,
Nao nyuki wakifika, wabaki kulialia.

Maua jana wacheni, humo mwake bustani,
Msiyatie mkononi, wala uzuri nyweleni,
Uzuri wa mlangoni, hupendeza kwa wageni.

Maswali

31. Shairi hhili lina beti ngapi?_____
    (a) Tatu
    (b) Sita
    (c) Nne
    (d) Nane
    (e) Tisa

32. Kila ubeti wa shairi hhili una mishororo_____
    (a) Miwili
    (b) Kumi na mbili
    (c) Mitatu
    (d) Minne
    (e) Sita

33. Shairi lote linahusu nini?_____
    (a) Watu wapendao maua
    (b) Wadudu
    (c) Wageni wapendao maua
    (d) Maua
    (e) Mvua

34. Mashairi yanayokuwa ya mistari mitatu mitatu huitwa
    (a) Tarbia
    (b) Tathilitha
    (c) Takhmisa
    (d) Utano
    (e) Mizania

35. Ni ubeti upi wenye vina vya kati “ni” na vya mwisho ni ni pia._____
    (a) Wa kwanza
    (b) Wa pili
    (c) Wa nne
    (d) Wa sita
    (e) Wa tano

SEHEMU D: UTUNGAJI

Umepewa insha yenye sentensi tano (5) zilizoandikwa bila mtiririko wa mawazo. Zipange ili ziwe na mtiririko wenye mantiki kwa kuzipa herufi A,B,C,D,na E katika nafasi za majibu.

36. Nilipofika darasa la tano sikuamini kama ningemaliza shule ya msingi kwani masomo yalikuwa magumu ……..
37. Sasa naanza kufikiria jinsi ya kujiunga na elimu ya sekondari……
38. Nilipokuwa mdogo, nilikuwa natamani sana nianze shule ili nikajifunze mengi nisiyoyajua……
39. Lakini kama muujiza, sasa namaliza darasa la saba……
40. Ndoto yangu ilikuwa kweli pale mama aliponipeleka shule kuanza darasa la kwanza……..

SEHEMU E: UFAAMU

Soma barua ifuatayo na kisha ujibu maswali 41-45 kwa ufupi

Shule ya msingi sotendungu,
S.L.P 8765,
Songambele.
27.07.2012

Kwako mama mpendwa,

Salamu nyingi zikufikie hapo ulipo. Je wote hamjambo hapo nyumbani? Mimi ni mzima wa afya na naendelea vema na masomo yangu. Wasiwasi wangu ni kwenu nyinyi mlio mbali na upeo wa macho yangu. Endapo wote ni wazima, furaa iliyoje kwangu.

Nina furaha kubwa kukutaarifu kuwa nimefaulu vizuri sana. Nimekuwa wa kwanza katika mtihhani wa darasa la tatu, muhula wa kwanza. Mama naomba umkumbushe baba kuhusu ahadi yakae ya kuninunulia baiskeli. Naahidi pia kufanya vizuri katika mtihani ujao.

Wako mwanao
Amina Said

Maswali

41. Mwandishi wa barua hii ni _____
42. Mwandishi aliiandika barua hii lini?_____
43. Lengo la barua ni nini?_____
44. Mwandishi anasoma darasa gani? _____
45. Hii ni aina gani ya barua? _____